**JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MKUTANO WA WASHAURI WA MIFUGO WA MIKOA NA WAKUU WA IDARA ZA MIFUGO NA UVUVI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

**UKUMBI WA KAMBARAGE JENGO LA HAZINA,**
**DODOMA TAREHE 17 JANUARI, 2022**

**Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi;**

**Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa (Mb) - Waziri wa Nchi OR - TAMISEMI;**

**Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega (Mb), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi;**

**Mheshimiwa Anthony John Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;**

**Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;**

**Bw. Emmanuel Tutuba - Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango**

**Prof. Riziki Shemdoe Katibu Mkuu - OR TAMISEMI;**

**Dkt. Rashid Tamatamah, Katibu Mkuu, Sekta ya Uvuvi;**

**Ndugu Tixon Nzunda, Kaimu Katibu Mkuu, Sekta ya Mifugo;**

**Dkt. Fatuma Mganga, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma;**

**Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi za Wizara mliopo hapa;**

**Ndugu Washauri wa Mifugo wa Mikoa na Wakuu wa Idara za Mifugo na Uvuvi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;**

**Kamati ya Ulinzi na Usalama;**

**Ndugu wanahabari;  Brassband;**

**Wafugaji especially Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji;**

**Mabibi na Mabwana.**

**"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"**

**Heri ya Mwaka Mpya 2022**

Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uzima na afya iliyotuwezesha kukutana hapa leo. Aidha, nakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi, pamoja na Uongozi wa Wizara kwa kunialika kushiriki katika ufunguzi wa mkutano huu. Vilevile, napenda kuwashukuru wote walioshiriki katika maandalizi ya kikao hiki cha siku mbili na ninyi nyote mliohudhuri.  Nafurahi kuona wadau tuko wengi sana ikiwa pomoja na Jr!

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi Wote,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Sekta ya Mifugo ni moja ya sekta muhimu za kipaumbele kwa Serikali yetu inayoongozwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Mwaka 2019/20 inaonesha kuwa asilimia 33 ya kaya zote hapa nchini sawa na watu milioni 14.6 (sehemu kubwa zikiwa familia za kipato cha chini), zinajishughulisha na ufugaji sambamba na shughuli zingine za kiuchumi. Hii inadhihirisha kuwa sekta hii ina mchango mkubwa katika kuwainua wananchi kutoka katika lindi la umaskini kwa kutoa ajira na fursa mbalimbali. Vilevile, sekta hii huchangia usalama wa chakula, na upatikanaji wa lishe bora na malighafi katika viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya mifugo hususani viwanda vya nyama, ngozi na maziwa. Aidha, biashara ya mifugo na mazao yake, ndani na nje ya nchi, pia huchangia katika kuipatia nchi fedha za kigeni na kuongeza kipato kwa familia zinazojishughulisha na ufugaji. Kwa sababu hizo, mkutano huu una umuhimu wa pekee kwa Taifa. Lakini pia, kwa wasiofahamu, mimi binafsi ni mdau wa sekta ya mifugo kindakindaki! Ni mfugaji mdogo wa ng’ombe, punda, mbuzi, kondoa, sungura, kuku/kanga/njiwa, nyuki na samaki!

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi Mliopo,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Kama Waziri wa Mifugo na Uvuvi alivyotuambia, nchi yetu ni ya pili barani Afrika, ikitanguliwa na Ethiopia, kwa kuwa na mifugo mingi. Idadi ya ng’ombe kwa mwaka 2019/20 ilifikia milioni 33.9; mbuzi milioni 24.5; kondoo milioni 8.5; na kuku milioni 87.7. Kutokana na taarifa ya hali ya Uchumi ya mwaka 2020, Sekta ya Mifugo ilikua kwa asilimia 5.2 ukilinganisha na asilimia 5.0 mwaka 2019. Ongezeko hili limechangiwa na sera inayolenga kuongeza uzalishaji wa kibiashara wa mifugo ili kukidhi masoko ya ndani na nje, kuongeza kipato cha wafugaji na kuboresha hali ya maisha ya wafugaji.

Hata hivyo, ongezeko hilo la idadi ya mifugo haliakisi mchango wa Sekta hii kwenye Pato la Taifa ambapo kwa kipindi cha miaka mitano (2015- 2020), mchango wake ulikuwa ni wastani wa asilimia 7 tu. Kiwango cha umasikini katika mikoa yenye mifugo mingi kama vile Mwanza, Simiyu, Manyara na Tabora kilikuwa zaidi ya asilimia 30, ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 26.4. Miongoni mwa sababu zinazopelekea mchango mdogo wa sekta hii katika Pato la Taifa na kurudisha nyuma jitihada za kupunguza umaskini ni pamoja na

kuendelea kwa utamaduni wa ufugaji wa kienyeji ambao hauzingatii ubora bali idadi kubwa ya mifugo, hali inayopelekea uwezo mdogo wa kukabiliana na magonjwa ya mifugo, upungufu wa malisho na uharibufu mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji na hatari ya kuenea kwa magonjwa ya mifugo na yale ambayo yanaambukiza binadamu. Sababu nyingine kubwa ni kukosekana kwa huduma za kutosha za ugani. Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Mwaka 2019/20 inaonesha kuwa ni asilimia 9.1 tu ya wafugaji wote ambao walipatiwa huduma za ugani katika kipindi hicho ukilinganisha na asilimia 55 katika kipindi cha Sensa ya 2007/08.

Kutokana na dosari hizo, tija katika sekta hii ya mifugo hairidhishi kabisa. Kwa mfano, uzalishaji wa baadhi ya mazao ya mifugo hususan maziwa kwa sasa bado upo chini hasa kwa ng'ombe wa asili ambao ndio wengi. Takwimu zinaonyesha kuwa, uzalishaji ni wa wastani wa lita 2 hadi 3 tu kwa ng'ombe kwa siku na nyama ni wastani wa kilo 150 kwa ng'ombe (*carcass weight*). Hiki kiwango kipo chini mno! Mimi naamini, endapo wataalam na wadau wa Sekta mtashirikiana kwa pamoja mtaweza kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa hadi kufikia wastani wa lita 20 hadi 30 kwa ng'ombe kwa siku na kuzalisha ng'ombe mwenye uwezo wa kutoa nyama kilo 300 hadi 400 kwa ng'ombe mmoja.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi Wote Mliopo,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Serikali kupitia Ilani ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025 ibara ya 40, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/22 – 2025/26) na Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipolihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma, tarehe 22 April 2021 imeweka wazi mwelekeo na malengo ya Sekta ya Mifugo kwa miaka mitano ijayo. Wengi wenu mnayafahamu hayo. Hivyo, naomba niwakumbushe mkayafanyie kazi malengo hayo ili kuiwezesha Sekta ya mifugo kutoa mchango unaostahili katika uchumi wa Taifa.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Huduma za ugani ni kiungo muhimu katika kuwasaidia Watafiti na Wafugaji kufanya uzalishaji wenye tija. Imeelezwa hapa wapo wafugaji wengi lakini ni maskini hawajui namna bora ya kufaidika na uwekezaji wanaoufanya. Hivyo, mchango wenu ninyi Washauri wa Mifugo utasaidia kuongeza pato la Taifa na kuboresha maisha ya wafugaji iwapo mtatekeleza majukumu yenu kikamilifu ya

kuwahudumia wananchi katika maeneo yenu ya kazi. Nitoe rai kwenu kujenga ushirikiano mzuri na madhubuti baina yenu na wafugaji mnaowahudumia.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi Wote,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Serikali inatambua changamoto mbalimbali zinazokabili utoaji wa huduma za ugani hapa nchini ikiwemo upungufu wa maafisa ugani, uhaba wa vitendea kazi (kama usafiri, *extension kit* n.k) na rasilimali fedha. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali ya awamu ya sita inaendelea kufanya juhudi kubwa kutatua changamoto hizi. Miongoni mwa juhudi hizi ni pamoja na kutoa mafunzo rejea kwa wafugaji na kuwajengea uwezo Maafisa Ugani, kujenga mfumo wa Ugani Kiganjani na kununua vyombo vya usafiri na vitendea kazi. Kwa nafasi hii ninatoa shukrani za pekee kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa uamuzi wake wa kuhakikisha wafugaji wanafikiwa na kupata huduma za ushauri wa kitaalam kwa wakati na ufanisi kwa kuidhinisha ununuzi wa **pikipiki 300** kwa ajili ya huduma za ugani. Pikipiki hizo ni sehemu ya nia aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha wafugaji wanapata huduma bora ili kuongeza tija katika ufugaji.

Hata hivyo napenda niwakumbushe kuwa, kazi hii ya kuwawezesha Maafisa Ugani kwa kuwapatia vitendea kazi ni jukumu la wadau wote katika Sekta ya mifugo. Hivyo, ninaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri, Miji, Manispaa na Majiji kutenga bajeti kwa ajili ya utatuzi wa changamoto zinazowakabili maafisa ugani katika utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, ninatoa rai kwa maafisa watakaokabidhiwa pikipiki hizo, kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na kuzitunza ili zitumike kwa muda mrefu na kuleta matokeo yaliyotarajiwa. Aidha, Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wahakikishe pikipiki hizo zinawekewa mafuta na kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara kulingana na mahitaji.

***Mheshimiwa Waziri, Ndugu Viongozi,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara katika sekta ya Mifugo. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetoa unafuu wa kodi kwa lengo la kuchochea zaidi uzalishaji, uchakataji na usindikaji wa mazao ya mifugo. Unafuu huo ni pamoja na:

(i) Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya asilimia 18 kwenye matenki maalum ya kubeba na kusafirishia maziwa na vifungashio vinavyotumiwa na wasindikaji wa maziwa kwa joto la juu yanayodumu muda mrefu (UHT Milk);

(ii) Kuondoa ushuru wa forodha wa asilimia 25 kwenye malighafi inayotumika katika usindikaji wa ngozi, mashine na vipuri vya kuzalisha viatu vya ngozi;

(iii) Kubadilisha tozo ya uuzaji nyama nje ya nchi kutoka Shilingi 150 kwa kilo ya nyama ya ng'ombe na Shilingi 50 kwa nyama ya mbuzi na kuwa shilingi 70,000 kwa kibali kwa pamoja; na

(iv) Kubadilisha tozo ya asilimia 1 ya thamani ya mzigo wa nyama inayouzwa njie ya nchi na kuwa Shilingi 40,000 kwa kibali.

Kwa kuzingatia maboresho hayo, watendaji katika ngazi mbalimbali za Serikali wanapaswa kuhamasisha na kusaidia Sekta binafsi kuwekeza katika Sekta hii ya Mifugo.

***Mheshimiwa Waziri, Ndugu Viongozi,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Sekta ya Mifugo ina uhusiano wa karibu na masuala ya mazingira hususan mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha uhaba wa maji na malisho, na hivyo kuchochea migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Mathalani, kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi, wafugaji katika baadhi ya maeneo, hulazimika kuhama na mifugo yao kutoka eneo moja kwenda lingine na hivyo kuchangia kwenye migogoro ya ardhi ambayo imeshajitokeza katika maeneo mengi ya nchi yetu. Napenda nitumie fursa hii kuwahimiza watendaji wa Serikali katika ngazi zote kutoa elimu na kusimamia ufugaji kwa utaratibu wa kuingiza mifugo katika maeneo kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza migogoro hii.

Aidha, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zisimamiwe kikamilifu ili kuepuka uharibifu wa mazingira na athari zake. Kumekuwa na uharibu mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji, mathalani, uchomaji wa misitu hovyo kutokana na shughuli za ufugaji kwa nia ya kupata malisho na nyingine nyingi zinazoambatana na jamii husika na ufugaji. Ili kufanikisha suala hili, Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina budi kubainisha, kutenga na kupima maeneo ya malisho na kuyaendeleza kwa kuzingatia Mwongozo wa Upatikanaji, Uendelezaji na

Usimamizi wa Maeneo ya Malisho wa Mwaka 2021 na kwa kuweka mikakati thabiti ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi Wote Mliopo,***
***Mabibi na Mabwana***

Matarajio yangu ni kuwa mtatumia vizuri siku ya leo na kesho kujadili na kuweka maazimio na mipango kazi ya utekelezaji kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuizingatia katika mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Mipango na Maazimio hayo yalenge kutatua changamoto zinazowakabili wafugaji na hivyo kuiwezesha Sekta ya Mifugo kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa na maendeleo ya watu. Napenda kusisitiza kuwa mipango na mikakati mtakayokubaliana katika kikao kazi hiki isiishie katika maandishi badala yake ionekane katika utekelezaji ili kikao hiki cha siku mbili kiwe na manufaa kwa sekta yetu ya mifugo na Taifa kwa ujumla.

***Mheshimiwa Waziri, Ndugu Viongozi,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kupendekeza kwenu mambo ambayo mimi naamini kuwa yakifanyiwa kazi na kusimamiwa vizuri, sekta ya mifugo nchini itapaa. Sekta ya mifugo na uvuvi ni muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sekta hii imejaa fursa. Kila penye mifugo maana yake pana chakula, ajira, biashara na kipato kwa wananchi. Hata hivyo, ili sekta ya mifugo iweze kukua, kutoa mchango mkubwa zaidi kwa Taifa na kuwezesha wafugaji na wananchi kwa ujumla kutumia fursa hizo ili kuboresha maisha yao, tunahitaji kuweka mfukumo mkubwa katika kuimarisha huduma za ugani na huduma mwambata katika maeneo yafuatayo:

(i) Usimamizi wa Maafisa Ugani: sambamba na ahadi na jitihada za Serikali kusomesha na kuajiri Maafisa Ugani na kuwapatia vitendea kazi, lazima kuanzia sasa kazi zao zisimamiwe ipasavyo. Itapaswa kila Afisa Ugani kuwa na orodha ya wafugaji anaowahudumia, ratiba ya kuwatembelea wafugaji ili kuwashauri na kufuatilia maendeleo ya mifugo, na kupima matokeo ya huduma anazotoa. Maafisa Ugani wasikae maofisini. Hata mavazi yao yafaa yawe ya Uwandani (Field). Mimi niko Zuzu, Mayamaya: nafuga sehemu zote mbili lakini sijawahi kutembelewa na Wataalam isipokuwa pale tu nilipowatafuta ninapokuwa na shida!;

(ii) Kuanzisha mashamba darasa na mashamba ya mfano ya malisho katika Vijiji na Halmashauri za Wilaya; mifano ya aina ya malisho ni pamoja na jamii ya kunde, nyasi au miti ya chakula kikavu cha mifugo. Aidha, Maafisa Ugani wenyewe wajitahidi kufuga kitaalamu kwa vitendo sio nadharia tu; * Asilimia 15 ya mapato yapelekwe kwenye kujenga miundombinu ya mifugo na mfuatilia na kutolea taarifa kila ½ mwaka;

(iii) Uzalishaji na uchakataji wa chakula bora cha mifugo; na uchimbaji wa malambo ya maji kwa ajili ya mifugo. Naamini SIDO, Taasisi za Teknolojia na Halmashauri wanaweza kutusaidia kama wataweka nguvu zaidi katika shughuli hizi. Hivi kweli Halmashauri haziwezi kuchimba malambo kutega maji wakati wa mifugo;

(iv) Kunenepesha mifugo na kuendeleza malisho (on-farm fattening and feedlot development);

(v) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ya mifugo ikiwa ni pamoja na madawa, chanjo na majosho ili kuzuia vimelea;

(vi) Kufundisha wafugaji kuhusu uchaguzi wa madume na majike ya mbegu (selection and cross breeding of local animals) ili kukuza kizazi bora cha wanyama wa asili au chotara na kuweka kumbukumbu ya upandishaji (breeding recording);

(vii) Kuimarisha na kueneza huduma ya uhimilishaji (artificial insemination);

(viii) Kuimarisha udhibiti wa biashara ya chanjo na madawa ya mifugo ili kuhakikisha yana ubora na bei zake zinaendana na uwezo wa wafugaji wadogo; kuzuia uuzaji wa chanjo na madawa yaliyoisha muda wake; na upatikanaji wa chanjo na madawa ya mifugo katika Vijiji na maeneo ya wafugaji na kudhitibi uuzaji/wizi wa dawa za ruzuku;

(ix) Kutafuta masoko ya mifugo ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo; na

(x) Kupanga matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo na kilimo cha mazao. Utekelezaji wa Mipango miji iko nyuma ya hali halisi on the ground!

- Kibali cha kuajiri Maafisa Ugani - Wasilisha maombi OR-Utumishi na mimi nitawaunga mkono

***Mheshimiwa Waziri, Ndugu Viongozi,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Baada ya kusema hayo, napenda sasa kutamka kuwa **kikao kazi cha Washauri wa Mifugo wa Mikoa na Wakuu wa Idara za Mifugo na Uvuvi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kimefunguliwa rasmi.**

Nawatakia majadiliano mema na nitafurahi kupata muhtasari wa mambo mtakayoyajadili na kukubaliana.

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…..***

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**